(02 BOOK)
I PART

(WHY BUDDHISM ?)

KWA NINI UBUDHA?

LENGO LA UBUDHA

"Niko huru,Bhiku,kutokana na minyororo yoyote ya mwili au ya roho.Ninyi pia,bhiku,muko huru kutokana na minyororo yoyote ya mwili au roho.Nendeni,enyi Bhikhu,kwa faida ya wengi,kwa furaha ya wengi,kwa kuionea huruma dunia,kwa faida ya miungu na binadamu,wawili wasiende njia moja. Hubirini enyi Bhikhu,Dharma ambayo ni nzuri mwanzo,nzuri katikati,na nzuri mwisho,ilivyoandikwa pamoja na lengo lake. Wapo viumbe ambao vumbi iliyopo katika macho yao siyo nyingi sana,na ambao wasipoisikia Dharma wataangamia.Hao ndio ambao wakiisikia Dharma wataielewa."

UTANGULIZI(foreward)

Ni kwa furaha kubwa nimekisoma hiki kijitabu kidogo cha Ubudha.Karibu kila sentensi inauangaza moyo uliojaa majonzi wa msomaji.Kinatoa majibu ya uhakika lakini mafupi kwa hasa maswali mawili..Kwa nini kuna dini?Na kwa nini kuna Ubudha?Kurasa zinatoa picha nzuri ya Ubudha,na picha yenyewe sio tu maoni binafsi ya mwandishi.Kila unapozidi kukisoma ndio mambo mapya yanadhihirika katika akili yako ya kidadisi.Mawazo yana mpangilio mzuri na yamejaa ukweli. Uzoefu mkubwa wa mwandishi huyu kama Kadhi Mkuu wa Ubudha wa Malaysia,na maisha yake marefu ya usomi na utakatifu kama mtawa wa Kibudha maarufu sana ni ambazo amezistahili sana kuandika kijitabu hiki chenye faida na chenye mafunzo kwa ufupi namna hii.Swali la "Kwa nini Ubudha ?" linajibiwa vyema hapa.

Dikwela Piyananda,
Maskani ya Kibudha
5017,16th Street N.W.
Washington D.C.20011,U.S.A.

MISINGI YA DINI

Kabla ya kulijadili somo la "Kwa nini Ubudha?",lazima kwanza tuulize mawazo ya binadamu kuhusu dini yalianza vipi.
Maelfu ya miaka iliyopita wakati binadamu alipoanza kufikiria mabo mbali mbali yaliyokuwa yakitokea katika mazingara yake,aliona mambo mengi ya kushangaza.Alishuhudia maafa na matukio mabaya ,ambayo yalileta woga,wasiwasi,hali ya kujiona kwamba hayuko salama,wahaka na mateso.Halafu akaanza kufikiria jinsi ya kutafuta ufumbuzi wa kuiondoa mikasa hii kutoka kwenye maisha yake.Lakini alifahamu kwamba haya mambo yapo nje ya uwezo wake wa kuyaelewa.Kwa hiyo alifikiria kwamba zipo nguvu fulani ambazo hazionekani,nguvu kubwa kuliko uwezo wa

binadamu,viumbe vilivyokuwa vinasababisha mambo haya.Akaanza kusali na kuziabudu hizi nguvu alizozitaswiri.Akaanza kutoa sadaka ya wanyama ili kupunguza nguvu za hasira.Akatoa shukrani mambo mengine yalipomwendea vizuri, akaamini kuwa vilikuwa ni vitendo vya mungu.Lengo la mambo haya,kwa hiyo,lilikuwa ni kupata ulinzi na kubarikiwa na maisha ya fanaka,na ambayo hayana matatizo mengi.Hivi ndivyo imani na matendo ya kidini yalivyoanza na kwa nini mtu wa kale alianza kusali.Hii dhana ya mwanzo ya dini ilipoendelea,mambo mengine muhimu yakajumuishwa,kama vile ibada na sikukuu za kidini.Hizi ziliendelezwa kufuatana na mila na desturi za maeneo na nchi tofauti.

Kwa hiyo msingi wa dini ulikuwa umewekwa na binadamu kama njia ya kumlinda kutokana na uoga mkubwa aliokuwa nao,hali aliyokuwa nayo ya kujiona kwamba hayuko salama,na kushindwa kuelewa mambo yaliyokuwa yakitokea kwenye mazingara.Kwa hiyo ni uoga wa kibinadamu ndio ulikuwa matofali ya kujenga dini.Hii ilikuwa siyo tu msingi wa dini zote,lakini ilikuwa ndio msingi uliotoa vitu kama matofali,mawe mchanga na simenti iliyohitajika kujenga jengo.

Ni pale imani ilipoanzishwa ndiyo iliwezesha jengo linaloitwa dini kukamilika.Imani pamoja na kuanzisha sadaka,sala,viapo,adhabu,toba,maadili-yote katika jina la Mungu.Pia ilikuwepo ahadi ya pahali pa amani ya milele panapoitwa paradiso ili kuwamiliki wanadamu

MSINGI WA UBUDHA

Baadaye tutakapojifunza dini inayoitwa Ubudha,tutaona kwamba Budha hakuzitumia hizo imani za zamani Hakuleta dhana ya Mungu au nadharia ya roho,au moto wa milele au mbingu ya milele kuujenga Ubudha.Hakutumia woga, au maoni yaliyopotoka kuhusu matukio ya maumbile kuiendeleza dini yake.Wala hakutaka watu waamini kama wapofu au wawe na ibada zisizokuwa za lazima.Hakuamini katika mtu kujitesa,au kuweka adhabu au amri katika kuujenga Ubudha.Zaidi ya hayo, hakudai kwamba amepata ufunuo wowote.

Alitumia mbinu tofauti kabisa kama vile ufahamu sahihi wa maisha,na dunia, na jinsi matukio ya kimaumbile yanavyotokea au utaratibu wa mbingu,hali halisi ya akili na vitu,na nguvu zilizopo,na jinsi ya kuishi kwa maadili na kujiendeleza kiroho,nidhamu,kuiendeleza akili,elimu,hekima na mwangaza,kama ndio vitendea kazi vya kulijenga hili jengo la dini. Ni kweli kwamba aliazima mambo fulani yaliyokuwa yakitumika na wanadini wa wakati ule,kama vile Dharma-njia sahihi ya maisha,karma-taathira ya vitedo vya mtu,Punabawa-kuzaliwa upya na maadili mengine,lakini sio kwa njia ile ile au kwa maana ile ile.Aliziboresha na akazitumia kufuatana na mantiki,sayansi na saikolojia,

DINI HURU

Ubudha siyo mkusanyiko wa dini tofauti,una tabia zake za kipekee.Baada ya kuelewa kwamba hakuna mwalimu mwingine aliufahamu ukweli wa juu au wokovu wa mwisho

wa binadamu,Budha alieleza kwamba hawa watu walikuwa wameendeleza tu uwezo fulani wa kidunia na waliweza kupata maendeleo kiasi tu ya kiroho na siyo utakaso kamili wa akili au mwangaza.Walimu hawa,kwa hiyo,walikuwa hawako huru na imani za ushirikina,mambo yasiyokuwa ya utakaso,kuhadaika,taaswira potofu,kuona maluweluwe na ujinga.Lakini 'dini' maana yake nini hasa?

Maana hasa ya dini inaweza kueleweka iwapo tu tutazama Budha alivyoianza njia yake tukufu ya kidini. Kama tukitumia neno 'dini'kuyaita mafundisho ya Budha,lazima pia tuelewe wanadini wengine wanalitumia hili neno vipi.Halatu tutaelewa kwa nini Ubudha unahitajika.

HAKUNA DOGMA

Budha alifanikiwa kuyaondoa mambo fulani ya upotofu yaliyoaminiwa na watu kwa maelfu ya miaka.Kwa mfano,katika siku za zamani kila mtu alikuwa akiamini kwamba jua lilikuwa likiizunguka dunia.Watu waliishikilia imani hiyo kwa sababu walikuwa hawafahamu sayari zilivyojipanga.Lakini baada ya Nicolaus Corpenicus ,mnajimu wa Poland kugundua na kuthibitisha kwamba jua lipo katikati ya sayari tunazoishi,hapo ndipo watu wakaanza kuuelewa ukweli wa nadharia yake na pole pole wakaiacha ile imani yao ya zamani.

Lilikuwepo jambo lingine kuhusu dunia ambalo watu walikuwa hawalielewi.Kwa maelfu ya miaka watu waliamini kwamba dunia ni tambarare.Halafu akaja Galileo Galilei mnajimu maarufu wa Italia ambaye alithibitisha kwamba dunia haikuwa tambarare,isipokuwa duara.Lakini nadharia yake ilipingwa sana na Kanisa,na Galileo aliitwa kwenye mahakama ya kanisa na alilazimishwa kuutubu usemi wake.Ni baadaye tu ndio watu waliukubali ukweli alioufundisha.

Mpaka kufikia karne ya 19,wanafalsafa waliamini kwamba atom ndio sehemu ndogo kabisa ya vitu ambayo haiwezi kumegwa.Lakini nadharia yao iliachwa wanasayansi walipofaulu kuipasua atom.Pia wako wanafalsafa waliokuwa na imani kwa maelfu ya miaka roho ilikuwa ni kitu ambacho kinadumu milele ambacho kimeundwa na Mungu,lakini Budha akasema hiyo siyo kweli.Lakini hii imani bado inadumu katika akili za watu,kama vile watu wanavyouona upinde wa mvua na kufikiria upo kweli.Budha alieleza kwamba dhana ya roho imepotoshwa na akili ya binadamu.Kama kweli ingekuwepo roho Budha angewaeleza wafuasi wake.Kwa sababu hii dhana ni ya muhimu sana kwa wanadini wote.

Nadharia ya Mwanzo wa Dunia kama ilivoelezwa na Charles Darwin ilikuwa inakanusha nadharia iliyokuwa ikifundishwa kwamba viumbe wameumbwa na Mungu.Jiolojia,Baolojia na Fiziolojia zilieleza wazi kwamba ilichukua mamilioni ya miaka kwa aina ya kwanza ya maisha kutokea dunianiHakuna upingano kati ya ugunduzi wa leo na mafundisha ya Ubudha.Ugunduzi kwamba vitu viliendelea pole pole,kwanza madini,halafu mimea na viumbe wengine, unawiana na mafundisho ya zamani ya Budha.

Kwa swali la jinsi maisha yalivyoanza Budha alitoa jibu rahisi na la mantiki.Alisema maisha ni muungano tu wa vitu na akili.Alisema akili inaundwa na hisia ,perceptions,yaani hisia zinazotumika kutenda kama vile miguu na mikono;mawazo na ufahamu.Vitu ni aina nne,vigumu,vya maji ,vya joto,vya hewa.Tunapoyatazama maelezo ya mantiki ya Budha kuhusu mbingu,tunaona anataja viumbe fulani vinavyoishi vyenye bahati na visivyokuwa na bahati,sio tu katika dunia hii lakini pia katika sayari nyingine.

Wanasayansi na wanajimu wameiweka akili wazi kuhusu uwezekano wa kuwepo viumbe kwenye sayari nyingine

Dini nyingi za zamani na imani nyingi za zamani ziko sawa na imani za kabla ya sayansi kuanza.,kuhusu muundo wa mbingu na mwanzo wa maisha.Lakini mafundisho ya Budha ,ingawa pia ni ya zamani,yanafanana na ugunduzi wa siku hizi.Lengo muhimu la Budha ni kumkomboa binadamu kutokana na minyororo ya utumwa wa kidini Taathira yake katika maisha ilikuwa kubwa sana. Imani iliyokuwa ikidumu kwamba tambiko ni muhimu sana kwa wokovu wa mtu ilikanushwa na Budha. Yeye alieleza kwamba kukuza maadili na kuitakasa akili ndio mambo muhimu kuliko yote kwa kufikia wokovu wa mwisho.Alieleza kwamba ili mtu awe na dini lazima aishi maisha ambayo hayana madhara,ya heshima,ya thawabu na yaliyotakasika.Lile tendo tu la kufanya tambiko au kusali peke yake haliwezi kumfanya mtu awe na dini,au kumwezesha kukamilika na kuokoka.

Pia aliwashauri watu kuacha vitendo viovu. Uovu unatakiwa kuachwa kwa faida ya viumbe wote,sio kwa ajili ya kumuogopoa Mungu au kuogopa adhabu.Pia alishauri tuendeleze tabia za kiutu,kutenda matendo mema,kuwasaidia wengine bila kuwa na sababu zozote za kibinafsi.

Budha .alitushauri tusiwe watumwa wa nguvu za nje ili tuziendeleze nguvu za akili zetu kwa kujiamini.

Pia alieleza kwamba binadamu ndie anayesababisha kila kitu katika dunia hii. Maumivu na raha yote yanasababishwa na binadamu mwenyewe,na binadamu anao uwezo wa kuyaondoa mateso yake.Binadamu anaweza kujifunza kudumisha amani na furaha kwa kutumia hekima bila kuchoka,bila kutegemea nguvu za nje. Ni akili ya mtu isiyikuwa na mafunzo ndiyo inayosababisha matatizo yote, balaa,vurugu,nuksi na migongano.Wakati huo huo binadamu anaweza kuigeuza hali ya balaa iliyopo duniani iwe ya amani,fanaka na mahali pa furaha kwa wote kuishi-kama tu akiitumia akili yake vizuri.Matatizo yaliyoletwa na watu lazima yatanzuliwe na mtu mwenyewe.Hii inawezekana iwapo tu tutazitakasa nguvu za akili.

KUKABILIANA NA UKWELI

Ubudha ni dini ambayo inamhimiza mtu kukabiliana na hali halisi bila ya kutegemea dhana za kubuni,na kuupokea ukweli popote pale utakapokuwepo.Ubudha haupingi ugunduzi unaohusiana na mambo ya dunia unaofanywa na wafikiriaji wakubwa na wanasayansi Ingawa Budha alitilia mkazo zaidi maendeleo ya kiroho,hakuyapuuzia maendeleo ya dunia.Mafundisho yake yalitoa ushauri mzuri unaoweza kufanyiwa kazi

wa jinsi ya kufanya kazi vyema bila kupoteza muda na juhudi,na jinsi ya kutenda mambo kwa hekima. Kwa maendeleo ya binadamu.Alisema kwamba mtu ni lazima atimize wajibu wake kwa familia yake,rafiki zake,nchi na dunia nzima.Kwa hiyo Wabudha hawatakiwi kuyapuuza majukumu yao kuifanya dunia hii kuwana furaha zaidi na ya amani. Kwa kutoa mchango wao kwa uwezo wao.Hakuziigilia shughuli zozote za serikali.

Lazima isemwe pia kwamba Budha hakutaka kuzitumia nguvu za kisiasa au za kijeshi kuiendeleza dini yake ,ingawa wafalme na mawaziri walikuwa mingoni mwa wafuasi wake wengi.

Hapa tunayo njia ya kidini ambayo inatufundisha kuwajali wengine,kujitolea mhanga maisha yetu kwa ajili ya binadamu wanaoteseka.Inatutaka tuzifuate kanuni za kidini au nidhamu kwa hiari,siyo kama amri ambazo tumepewa na viumbe ambao hawaonekani. Kwa kufuata kanuni nzuri ambazo sisi wenyewe tunaziamini,tunapata nafasi ya kujikamilisha na pia kuwasaidia wengine waishi kwa amani.

NJOO MUONE MATOKEO MARA MOJA

Kufuatana na dini hii tunaweza kuyaona matokeo ya matendo yetu mazuri au mabaya katika maisha haya haya tunayoishi. Starehe za mbinguni au starehe za nirvana tunaweza kuzipata katika maisha haya.Hakuna sababu ya kusububiri mpaka ufe.

Hii ndiyo maana Budha aliwakaribisha watu kuja kuiona njia yake ya kufundisha,sio kuja na kuamini mara moja.Aliwashauri watu jinsi ya kuchagua dini nzuri,kwa kuifikiria,kuichambua na kuitafiti kwa njia tofauti bila kukubali chochote kwa hisia na imani.Ni dhahiri kwamba kila dini inakuza imani.Lakini imani katika Ubudha sio kunyoosha mikono kwa vitu visivyoonekana,siyo kufanya mambo kwa ajili ya woga. Imani ya Ubudha ni kukubali mambo baada ya kuyachunguza kwa muda mrefu na kufanya uchambuzi sana.Hii ndiyo maana Ubudha unaitwa mafundisho ya kuchambua.Hii dini inao uchambuzi wa kisayansi na kisaikolojia ambao umewapendeza wasomi wa zama za sasa.

SHERIA ZA MBINGU

Kwa wale waliozungumza kuhusu chanzo cha kwanza cha dunia Budha aliwaambia kwamba haiwezekani kukifahamu chanzo cha kwanza cha dunia kwa kuwa kila kitu kinabadilika,vitu vinategemeana,na vinaathiriana.Kitu ambacho leo kinaweza kuwa chanzo,kesho kinaweza kuwa matokeo.Baadaye matokeo fulani yanaweza kuwa chanzo.Hali kama hiyo inaweza kuendelea tena na tena,bila kikomo.Hii ndiyo sheria ya annicca.,ya vitu kutokudumu.

Kuhusu kuanza kwa dunia yenyewe hakudai kwamba viumbe vyote vinamilikiwa na utaratibu wa Kibudha.,isipokuwa ni sheria ya mbingu.Mtu alikuwa anatakiwa kuikubali nafasi yake katika dunia,na vitu vyote,hai au sio hai.kuwa ni vimoja. Msomi Rhys David alisema'katika kila kiumbe,kiumbe chochote kile,mahusiano ya sehemu zinazokiunda yanabadilika kila wakati,kwa hiyo hakina sekundi mbili zinazofuatana.Inafuatia kwamba mara tu utengano ukitokea,hapo hapo kubomoka na kumeguka kunatokea,kwa vile

hakiwezi kuwepo kitu,bila vitu kuja pamoja;-vitu haviwezi kuwa bila kuwa tofauti;-vitu haviwezi kuwa tofauti bila kuanza kubomoka,na kumeguka,ambako baadaye kutakamilika":

Budha alikuwa mwalimu ambaye aliigundua hali hasa ya sheria za mbingu na aliwashauri watu waishi kwa kuzifuata hizi sheria.Alisema kwamba wale ambao wanazikiuka hizi sheria,na kuishi maisha maovu,kama vile kwenda kinyume na maumbile,wawe tayari kukumbana na matatizo.Haiwezekani kuzikwepa taahtira za kuzikiuka sheria za mbingu.Haiwezekani kuziepuka kwa kusali kwa Mungu,kwa sababu sheria hizi za mbingu hazina upendeleo.Lakini Budha alitufundisha jinsi ya ya kuziepuka taathira mbaya kwa kutenda mema zaidi na zaidi.,kwa kuizoeza akili na kuondoa mawazo maovu kutoka akilini.Baada ya kuivunja sheria ya mbingu ,hakuna njia ya kuiondoa taathira zake mbaya isipokuwa kwa kushirikiana na sheria hiyo hiyo ya mbingu.

Akili yetu lazima iwe na uwezo wa kufanya kazi bila kuchoka.Hata kama yapo matatizo gani lazima tuwe imara.Tuvumilie shida zote lakini tusitende uovu,hata kama tukipigwa bakora au mijeledi,hata tukiwekwa rumande,hata ikitubidi kukesha usiku.

Mtu ni lazima awe na tabia isiyo na lawama,pia awe haziogopi hatari za aina yoyote. Haitoshi kwa mtu kushinda hatari zote ikiwa anaishi maisha ya lawama Kwa sababu ukifanya mambo kama hayo ndiyo unakumbana na nyundo ya dola. .Halafu pia,kuna faida gani kama mtu maisha yake hawezi kulaumiwa lakini ni mvivu.?

Matatizo mengi yameifika nchi yetu. Vyeo vinauzwa. Ndio maana maovu mengi yanatokea,na hakuna mtu wa kuyarekebisha,hakuna mtu wa kuyakemeaSiyo hivyo tu,haya maovu yamekuwa kama ndio mtindo wa maisha.Mtu akifanya kosa na akishutumiwa,badala ya kujaribu kuonyesha kwamba hana hatia,anatafuta ikiwezekana washirika wenzake katika vitendo vyake vya jinai.Hii tabia itatupeleka wapi?

Ukiwadadisi watu utaona kwamba wanafanya makosa mengi sana.Wengine wanatumia ndumba na hirizi ili waweze kufanya uzinzi,,wengine wagoni,wengine walevi,wengine hodari wa kutukana,wengine wanatamani vitu vya watu wengine.;-nachelea kuendelea kwa sababu itanibidi kuwaumbua watu wengi,

Au niendelee sio? Kama ukiwachunguza watu wa dunia hii,ni makosa gani ambayo hautayaona?Kama ukiwachunguza wale wenye vyeo.Si utakuta kwamba wanafanya kazi tu ya kujinufaisha wenyewe?.Vyeo vinauzwa tu kama bidhaa ya sokoni,utaona wana husuda,chuki,majigambo,walafi na watumwa wa hela.

Wakati maovu kama haya yakitokea,tunaweza kutegemea kila aina ya balaa.Na ili ujue kwamba mambo haya yanaleta sana matatizo,ipo mifano mingi katika historia ya zamani.
Ni tabia ya maisha kwamba wanaadhibiwa wenye makosa na wasiokuwa na makosa.Hii tunaweza kuona hata katika vita za leo.

Kwa ajili ya mambo haya yote tujihadhari.Huzioni hizi vita zote?Huzisikii hizi balaa?Haujifunzi somo lolote kutokana na mambo haya?Mataifa na miji inamezwa na kuteketezwa,na watu wasio na idadi wanapoteza uhuru wao.

Kama moto wa milele hauwezi kutufumbua macho,basi haya matatizo yatufumbue macho Au utasema kwamba haya ni mambo ambayo hayajatokea?Watu imewafika adhabu kubwa sana,lakini adhabu yetu itakuwa kubwa zaidi ambao hatuwezi kufumbuka macho hata tunapoyaona matatizo yao.

Je,haya maelezo yanachosha?Labda yanachosha ,lakini tukiyazingatia,ipo faida fulani;-kwani lengo lake sio kusema maneno ya kufurahisha watu;;-siyo hivyo tu,lengo lake haliwezi kuwa hilo hata mara moja.Lengo lake ni kuwafanya watu wawe wanyenyekevu,wajirekebishe. Huu ndio unaweza kuwa msingi wa fanaka na maendeleo kwetu sisi.

NGUVU YA AKILI

Nadharia ya karma aliyoieleza Budha inakubaliwa na saokolojisti maarufu wa Switzerland,Carl Jung kama ‘akili ya wote’Hii si kitu kingine chochote kile bali ni mkusanyiko wa mbegu za vitendo vya karma katika nguvu ya akili. Iwapo akili ya wote na’ hamu ya kuishi’ ikibakia akilini,kama inavyoelezwa na wanafalsafa,watu watazidi kuzaliwa tena kama wanaamini au kama hawaamini.Sehemu za mwili zinaweza kubomoka,lakini akili pamoja na ‘dhamira ya kuishi’vitapelekwa kwenye maisha mengine kufuatana na akili ya wote au karma.

Nguvu ya uzito pamaoja na kuhifadhika kwa nishati kama ilivyogunduliwa na wanasayansi kama vile Newton,vinaunga mkono mafundisho ya karma.

Budha alifundihsa kwamba kama mtu ni mjinga,asitendewe ubaya au kulaumiwa kwa ujinga wake ili aelekezwe yale mambo asiyoyafahamu.

Watu wanaoichukia Dharma ndio wanaotenda uovu.;-kwa sababu itawezekana vipi kwa mtu anayefanya ufuska kiholela kama nguruwe,mtu anayependa fedha,mtu ambaye hataki maisha ya kadiri, kuishi maisha haya?

Watu wameufanya uovu kuwa kazi yao,huko ni kuifanya mioyo yao kuwa migumu,na inaonyesha kuwa kuna giza katika ufahamu wao.

Watu wanazidisha uchu. Wanao uwezo wa kudumisha kadiri wanapostarehe na utajiri wao,wanapofaidi vitu vizuri,wanapofanya mambo ya anasa.,lakini wanachagua kufanya mambo bila kutumia kadiri,na hii ndiyo inayowaharibu.

Wanafanya kila aina ya uchafu,siyo kama wanateleza katika vitendo vyao au wanafanya makosa kwa bahati mbaya,isipokuwa wanatumia mbinu wanapofanya vitendo hivi viovu.Wanafanya mambo ya uchafu,yaani,uzinifu,uzinzi,mapendo kinyume na maumbile,husuda na kila aina ya laana na ufuska.

Kuishi maisha ya kadiri ni jambo zuri ambalo mwisho wake ni mzuri.Kuzidisha anasa mwisho wake ni mbaya.Halafu watu wengine wameshaanza kuwa wazee lakini bado nao wanataka kuwa mabingwa wa ufuska.

Thawabu ni kama nguo kwetu.Nguo zinaufunika mwili,thawabu inaifunika roho.Roho isiyokuwa na thawabu itauletea mwili kila aina ya majeraha,kila aina ya balaa.

MTU ANAWEZA KUWA NA UWEZO MKUBWA

Maoni ya Ubudha ni kwamba binadamu ni kiumbe wa juu.Anawashinda hata deva,viumbe wa roho wanaoishi mbinguni.,kwa hekima na nguvu.Bodhisatva aliondoka mbinguni na akashuka duniani ili apate mwangaza wake.Kwa nini?Kwa vile deva hawana hekima au utakaso unaowezesha kufanikisha maendeleo haya ya juu kama vile kupata Mwangaza.Hali hiyo inaweza kufikiwa na binadamu tu.

Ubudha unampa heshima kubwa mtu anayeishi katika jamii ya binadamu Upekee wa binadamu kati ya viumbe wengine unatambuliwa,Uwezo wa kufanya marekebisho kwa hali mpya au mazingara ni uwezo ambao binadamu anao.Budha alitambua maendeleo ya maadili na hekima ya binadamu na akaonyesha njia ya kuyakamilisha.Kuzaliwa kama binadamu hakutokei hivi hivi tu.Kuwepo kwa binadamu kunatokana na matendo ya karma .Budha aliutambua umuhimu wa kuzaliwa binadamu.Hakuna kiumbe mwingine mwenye uwezo wa kufikiria kwa mantiki kama binadamu.Na huu ndio ukuu wa binadamu.

Uwezo wa binadamu ni mkubwa.Akili aliyonayo mtu inaweza kuendelezwa kwa kiasi kikubwa.Kufuatana na Ubudha,hahitaji kiumbe chochote cha kiroho kumsaidia.Yeye mwenyewe anao uwezo wa kuikamilisha elimu yake.Uchambuzi wa Budha kuhusu hili swala ulitolewa baada ya yeye kupata Mwangaza wake ambao aliupata bila msaada wowte wa nje wa kiroho.

Kufuatana na Ubudha mtu anaweza kuwa kama mungu kama akiishi maisha ya staha na thawabu bila kujali kama yeye ni dini gani.Lakini dini nyingine zinamshauri mtu kusali kwa Mungu ili apate baraka.Pia zinahuburi ni baada ya kufa tu ndio mtu anaweza kwenda mbinguni.Lakini maisha ya mbinguni hayatamwezesha mtu kuwa kama Mungu.Budha alisema kwamba binadamu wanaweza kuzipata starehe za mbinguni hapa duniani.wasipoitumia vibaya nafasi yao.Lakini dhana ya Ubudha ya mungu ni tofauti na dini nyingine.

HALI YA AKILI

Kubadilka haraka kwa akili na kwa mwili vyote vimeelezwa na Ubudha.Kufuatana na Ubudha,katika kila nukta,au hata kabla ya nukta,nguvu za akili zinatokea na kupotea. Baolojia,fiziolojia na saikolojia pia zinathibitisha kubadilika kwa maisha.Kwa hiyo maisha hayaishi kubadilika.

Saikolojisti mwingine maarufu,William James amezungumzuia jinsi akili inavyobadilika haraka.Alieleza kuwa mawazo yanakuja na kuondoka haraka.Kwa kutegemea kitu kilicholeta mabadiliko,wazo likizaliwa tu,hilo wazo linazaa wazo lingine,na lenyewe linakufa,Lile lilozaliwa nalo linazaa wazo lingine,nalo linakufa,inaendelea hivyo hivyo.

Kuhusu jinsi mawazo maovu yanavyoibuka akilini,jibu lipo katika dini ya Ubudha.Sababu ya uovu ni tabia ya ubinafsi ambayo inatokana na uchu.

Watawa wa Kibudha wanaishi maisha magumu sana ili wapate thawabu.Sisemi ni lazima uishi kama wao Ishi tu maisha yako ya kawaida,lakini,katika kila kitu ,usiwe mlafi.,kwa sababu hiyo ndio inayoleta matatizo.Kitu chochote kikitumiwa kwa ulafi ni makosa.Kwa sababu tazama inavyokuwa mtu akikasirika.,anasisimka,baadaye anaanza kutukana mwishowe anajeruhi watu.Na hivyo ndivyo ilivyo katika mambo mengine pia,katika kutafuta warembo,au vyeo,au kitu kingine chochote.

Na usinielewe kwamba watawa niliowazungumzia sasa hivi walikuwa na nguvu;-wengi walikuwa ni wadhaifu na matajiri na wanaishi maisha ya anasa kuliko wewe.

Lakini kwa nini naongea kuhusu wanaume?Wasichana pia wamefanikiwa kuwa watawa na wameishi maisha magumu ya kitawa.

.Hata hivyo,sitaki kubishana na wewe kuhusu hili swala kwa vile naona umeshaamua kwamba unataka kushindwa na wanawake.Lakini kama ipo kazi yoyote ambayo siyo ngumu,angalau ifanye hiyo kazi.Uthibiti mkono wa ujeuri na jicho la uasherati.Kuna kitu gani kigumu?Tenda haki na wema,usimkosee mtu yeyote,kama wewe ni tajiri au maskini,muuza duka au mfanyakazi wa kuajiriwa;-kwa sababu hata maskini wanatenda mambo ambayo siyo ya haki.Si unaona wanavyogombana sana na kugeuza kila kitu chini juu.

Kama huwezi kutoa zaka,basi angalau usimwibie mtu mwingine.Kama huwezi kufunga,basi angalau usiwe mlafi.Kama huwezi kulala kwenye sakafu ya simenti,au mahala pagumu,basi angalau usilale kwenye kitanda cha shaba,usitumie viti vilivyochongwa kwa meno ya tembo.

Ukitembea na vitu kidogo utakuwa huna kitu cha kuogopa,kutokana na kijicho au wanyang'anyi..Utajiri wako sasa umekuwa sio wa fedha bali ni utajiri wa mashaka. Umekuwa
tajiri kwa mashaka yako yalivyoongezeka maradufu

Sio lazima uwahudumie wqagonjwa lakini unaweza kumuagiza mtumishi wako awahudumie wagonjwa.

Tuone aibu kwa sababu tunashindwa hata na wanawake wanyonge.Katika mambo ya kidunia,kama vile vita au riadha tunawashinda,lakini katika mashindana ya kiroha ,mara nyingi wanatushinda.Sisi tunakuwa kama mbwa walafi ambao wanawaza chakula tu.Tunatakiwa kuwatawala,na sio tu kuwatawala ila kufanya hivyo kwa wema.

Kwa sababu yule anayetawala kwa jinsi hii pia anatakiwa kuongoza,yaani kuongoza katika thawabu;-lakini akipitwa katika thawabu,basi yeye sio mtawala tena.

Wanawake wanavaa vito,kwa sababu wanapenda kufanya hivyo ,na pia kuwapendeza wanaume.Ukiacha kuvichangamkia hivyo vitu,utawapunguzia gharama.

KILA KITU KIKO WAZI

Tunapojifunza kuhusu maisha na mafundisho ya Budha tunaona kwamba kila kitu kiko wazi kwa kila mtu.Hakuna mafundisho ya siri.Matukio yote katika maisha yake yalikuwa kama kitabu kilichokuwa wazi bila kufichika kitu chochote au matukio yoyote ya ajabu.Machoni pa Budha, mambo ambayo watu wengi waliyaita miujiza,yalikuwa ni mambo ya kawaida ya maumbile,isipokuwa tu mtu wa kawaida alikuwa anashindwa kuyaelewa.Kama vitu vyote vinafuata sheria tunaweza vipi kuiita miujiza?

KUENDELEA KWA MAISHA

Budha alieleza mtu anaanza maisha kama myama,halafu kuwa binadamu,kutoka kuwa binadamu anaishi maisha ya kiroho.-kutoka maisha ya kiroho anaishi maisha ya brahma,na kutoka maisha ya brahma kuishi maisha yaliyokamilika.Pia mtu anaweza kutoka kwenye maisha ya thawabu na kwenda kwenye maisha yaliyokamilika.Hali ya kinyume pia ilielezwa,kwamba mtu anaweza kutoka maisha ya binadamu na kuishi maisha ya mnyama.

MAISHA YA KADIRI

Dini zote zinahubiri mafunzo ya kuinusuru roho.;-kupita njia ya katikati;-kati ya kustarehe kupita kiasi na kujitesa kupita kiasi,ndio mafundisho ya UbudhaNjia ya kati kati ni kuacha kufikiria kwamba utaishi milele na kuacha kufanya mambo ambayo yanaweza kukuua mara moja.

Budha aliwashauri wati waifuate njia ya kati kati katika kila sehemu ya maisha yao.Lakini watu wengine hawajaelewa bado maana na faida ya njia hii ya kati kati.Maana ya kina ya njia hii sio tu kufuata maadili,au kuepuka itikadi kali,maana yake ni kuacha kuzitumia hisia zetu za mwili,kama vile,macho,masikio,kwa njia isiyofaa.Hisia zitumike kwa usalama wetu na usalama wa wale wanaotuzunguka.Hivyo,wote tutaweza kuishi kwa salama na amani. Dini zote zinaizoeza roho,lakini kwa bahati mbaya watu wengi wanayatumia maisha yao wakifukuzia kuzistaresha hisia.,na kuzitumia vibaya kukidhi hamu zao tu.Mwisho,uchu unakuwa mkubwa kiasi kwamba,huko kukudhi ndio inakuwa kazi pekee inayofanywa na akili.Mambo ya kifisadi yanafanyika,matendo ya ukatili,wazimu,mashindano kwa kutumia hila,migogoro ambayo imekuwa ni ya kawaida kabisa katika maisha yetu ya kisiasaChanzo chake ni akili isiyotosheka,ambyo inatokea kwa vile hisia zinatumika vibaya.Halafu uwezo wa hisia pole pole unafifia na matokeo yake viungo vya mwili vinafikwa na magonjwa mengi,Hivi ndivyo binadamu anavyolipa gharama ya kuziwekea mzigo mkubwa hisia zake.Kama starehe zikiendelezwa sana

katika dunia hii,hatutakuwa na muda wa kujitayarisha kwa maisha ya baadaye,au maisha yetu katika dunia inayofuata.

TABIA YA UPOLE

Budha alisema kwamba itakuwa ni ukatili na ukiukaji wa haki za viumbe kwetu sisi kmuua kiumbe oyote kwa sababu yoyote.lakini walimu wengi wa diniiwamelipuuzia hili swala la huruma.Kuteketeza maisha ya viumbe wengine sio njia pekee ya kuwazuia wasilete usumbufu.Ukweli ni kwamba ni binadamu ndio wanaoleta usumbufu kwa viumbe wengine.

Lengo la Ubudha sio kutengeneza taaswira zisizokuwa na maana katika akili,sio kuzipendeza tu hisia za binadamu au kuziendekeza hamu fulani za kidunia. Lengo ni kumwasha binadamu kuwa anaweza kupata furaha kwa kuyaelewa vizuri maisha na maumbile.

HALI HASA YA MAISHA

Lengo la maisha ni la mazonge mazonge sana kwa sababu kila mtu anatoa tafsiri yake.Lakini kufuatana na Ubudha lengo la kuishi ni kutafuta ufumbuzi kamili wa matatizo ya maisha na kupata furaha ya milele.Nadharia ya utabibu,sayansi na teknolojia bado havijapata ufumbuzi wa mateso ya akili ya binadamu,kukata tamaa.au hali ya kutotosheka na maisha.Lakini Ubudha unayaeleza mambo haya vizuri Mateso yanayo sababu,na pia furaha inayo sababu,

HEKIMA NI NINI?

Kwa maoni ya Ubudha,hekima ni kutaswiri vyema na kufikiri vyema,kuzielewa sheria za mbingu na kuendeleza ufahamu. Ufahamu maana yake sio tu kuuona ukweli,bali pia kuigundua njia ambayo inaweza kuleta wokovu kamili kutokana na hali yoyote yenye kasoro katika maisha.

Kwa hiyo,hekima ya kweli haiwezi kupatikana katika vyuo au katika maabara za utafiti,au hata sehemu ambazo watu wanaenda kusali au kufanya ibada.Hekima imo ndani ya akili yenyewe. Wakati uzoefu,utambuzi, na utakaso vimekamilika,hii hekima ambayo ndiyo ukamilisho wa juu kabisa, itaibuka na kuonekana. Lengo la maisha ni kuipata hii hekima.Badala ya kutafuta anga za juu,mtu lazima afanye juhudi ya kuzitafuta anga za ndani.

Mtu anaweza kuzishinda nguvu za kidunia zinazoweza kuzuia maendeleo yake kwa kuiimarisha na kuitakasa roho yake.Ndipo atafikia upeo wa juu wa furaha ambapo nguvu za uovu hazina uwezo wa kufanya kazi tena.

Kwa hiyo tusimame imara tufanye vitendo na pia tuvikamilishe.Askari anatakiwa sio tu atende jambo lakini pia alikamilishe,ili sio tu aue,bali asimame baada ya kuua.Kwa sababu wengi wameupata ushindi huu,lakini wakaanguka tena.Kwa sababu hata baada ya ushindi lazima tusimame.Adui anaweza kupigwa,lakini vitu vilivyopigwa vinajihuisha

tena tusiposimama.Lakini kama baada ya kuanguka vinasimama tena,iwapo tumesimama,basi lazima vitaanguka tena Ikiwa hatubabaiki basi mpinzani hawezi kusimama tena.Budha aliulizwa,"Wewe ni mtu wa amani.Lakini,kipo kitu chochote ambacho unaafiki kiuawe?' Akasema,"Naafiki hasira iuawe,Kila mtu aiue hasira yake"

Kwa hiyo tunapaswa kuwa na ngao ya tabia njema.Mtu yeyote anayeathiriwa na hasira,au ashiki,au anawania vitu vingi visivyo na faida,ajue kwamba vita ni ngumu.Fanya upelelezi kila upande,jizatiti vyema,imarisha boma lako.Ukishindwa katika vita utakuwa mateka wa adui.

Zile roho za kiovu za maadui zako zinazowaongoza kutenda uovu ndiye adui unayepigana naye..Sera zetu nzuri ndio silaha yako. Tuna imani kubwa sana na sera zetu,kwamba hata kama upo uovu kiasi gani,sera zetu zitaushinda huo uovu,sera zetu zitang'ara.Kwa hiyo tusimuogope adui,tuwe na sera nzuri.Vumilia shida zote.Hata ukikatwa na panga,vumilia ili ulifikie lengo letu.Lengo la adui sio kutushinda,ila kutudhalilisha ili tuifikie hali yake ya aibu.Ushindi kwake yeye ni kutuvurugia tu mafanikio yetu.

Kwa hiyo tupigane na tuvishinde vitu vyote vinavyoturudisha nyuma;-ghaghabu,ufuska,maringo.kila aina ya tamaa.

Hasira zako zisielekezwe kwa ndugu yako au kwa jirani yako;-hasira zielekezwe kwa chanzo cha matatizo yetu,muundo wa maisha usiokuwa na maadili,ambao haumjali binadamu.

Watumishi waheshimuni waajiri wenu.Fanyeni kazi bila kuwa wezi.Waajiri wasiongee na watumishi kwa lugha ya vitisho,wasiwe wakandamizaji.Sio tu watumishi wawe watiifu kwa waajiri wao,ila pia,watu mitaani waheshimiane,waishi kama ndugu.

Lakini labda kuna mtu atauliza kwa nini watu wengine wanakuwa watumishi,mambo kama haya ya utumishi yameingia vipi duniani?(na wengi najua wangependa sana kuuliza maswali kama haya,na kupata majibu yake)Utumwa unasababishwa na tamaa,kudhalilika na ukatili.Kwa nini,kwa mfano,lipo taifa moja Mashariki ya Kati ambalo limelifanya taifa lingine kuwa watumwa?

Ipo imani kule kwamba hii inasababishwa na mgomo kwa wazazi,kuhusu mababu zao wa zamani. Watoto wajihadhari sana,kila wanapokataa kutimiza wajibu kwa wazazi,ina maana kwamba wanastahili kuwa watumishi.Ndio ikawa kwamba,zilipotokea vita,wote wakachukuliwa mateka.

Kuhusu watoto na pia watumishi,wote wafundishwe dini.Watumishi wasiachiwe tu kunywa pombe ya machicha

Kwanza lazima tuwe na roho ya kishujaa,kwa sababu tunapaswa kujizatiti ndani,halafu nje.Halafu tusimame imara.Lazima ujue kwanza jinsi ya kusimama imara.Yule anayejifikiria amesimama ajihadhari asianguke.Sio kusimama vyovyote ila kwa usahihi.Watu wenye uzoefu wa vita wanafahamu jinsi ya kusimamaWapiganaji ngumi au

mielieke kwanza wanajifunza jinsi ya kusimama,na katika vita ndio muhimu zaidi kuliko hata katika mieleka

Mtu anayesimama vyema ni yule asiyesimama kivivu.Hata watu wenye thawabu wanaonekana kwa jinsi wanavyo simama wima Mtu wa anasa hasimami wima ila anajikunja,pia fuska na anayependa pesaYule anayejua kusimama kutokana na kusimama kwake,huo ndio unakuwa msingi wake wa kuyaondoa matatizo.

Simama,kwa hiyo,jifunge vizuri mshipi kiunoni Yaani fuska ni mtu abaye amelegeza mkanda wake,wewe usiwe hivyo,mkanda wako uwe mkanda wa Dharma Katika miguu yako vaa viatu vya kueneza sera zetu za amaniMawazo maovu yanaufanya mwili uugue.Ni mambo mawili yanayoufanya mwili wako uugue,mawzo maovu na mazingara machafu

NJIA AMBAYO INAWEZA KUFANYIWA KAZI

Filosofa mmoja ana maoni kwamba dini inapinga uzoefu wote wa binadamu,Kama hivyo ndivyo ilivyo,Ubudha sio aina ya dini kama hiyo.,kwa vile Budha amefundisha kila kitu kutokana na uzoefu wake mwenyewe

Filosofa wengi wameitumainia tu elimu yao ya kidunia na hekima yao.Kwa kuzifanya akili zao ziwe na nidhamu wameweza kugundua mambo mengi mapya.Lakini hata kwa kuitumia hekima hiyo,haiwezekani kuijua hali halisi ya vitu bila kuitakasa akili yako.

Tukiyachunguza maneno mengine ya hawa filosofa,tunaona ukweli kiasi katika maneno yaoLakini maneno yao mengine yanabakia kama falsafa kavu kwa vile wamezitumia akili zao tu,akili ambazo zilikuwa zimepumbaa.

Lakini Budha aliutumia ubongo wake no moyo wake;-kama hekima iliyoboreshwa ikiunganika na huruma.Kwa hiyo akapata hekima ya kuelewa jinsi vitu. vinavyohusiana na vitu vingine.Ndio maana mafundisho yake hayakuwa tu nadharia ya falsafa kavu,lakini yanabakia kuwa njia inayoweza kufanyiwa kazi,ya kutanzua matatizo ya dunia Lengo la dini ni kuwakomboa viumbe.Kwa hiyo kila dini ni laima ifanye juhudi kubwa kujaza upungufu wa mwanadamu kwa kutumia sayansi ya ufahamu wa kiroho na mafunzo ya maadili Dini haiwezi kutenganishwa na maadili.

DINI INAZUIA MAENDELEO YA BINADAMU?

Wanasayansi wengi,wafikiriaji wakubwa na wanafalsafa wameweka uhasama dhidi ya dini.Wanasema dini inazuia maendeleo ya mtu na inawapotosha watu kwa kuwafundisha imani na matendo yasiyokuwa na maana ya kishirikina na kuwafanya watu wasiuelewe ukweli wa sayansi. Lakini tukitazama wanavyoitafsiri dini,tunaona kwamba Ubudha haupo katika makundi hayo ya dini. Kwa hiyo hata kwa maoni yao hao hao wasomi,Ubudha ni dhahiri dini ya kisayansi na haiwezi kupuuziwa kuwa ni dini ya

kishirikina.Zaidi ya hayo,Budha hakuelezea tu ukweli wa binadamu,lakini pia ukweli wa juu wa kiroho,Kama kitu chochote ni kweli,basi kitabakia kweli daima.Kama kitu chochote kitabadilika,masharti fulani yanapobadilika,basi hakiwezi kuwa ukweli wa juu.Hii ndio maana ukweli kama unavyoelezwa na Budha ni ukweli mtukufu-ukweli unaomfanya mtu atukuke. Daima itabakia njia ya haki itakayoweza kustahimili changamoto ya sayansi au akili.Njia ya Budha ,kwa hiyo,haitingishiki.Na wasomi wataiheshimu,kama tu wataelewa Budha alifundisha nini.

DINI YA UVUMILIVU

Jambo ligine muhimu alilofundisha Budha ni jinsi ya kuishi,kufanya kazi na kushirikiana na wafuasi wa dini nyingine bila kubugudhi au kupuuzia shughuli zao.Hii njia ya uvumilivu ni muhimu sana ili tuweze kuishi kwa amani bila ubaguzi wa kidini,migongano na ugomvi.Mafundisho ya Budha ya amani na uvumulivu ni mafundisho mema.Uvumilivu ni tabia tukufu sana.Ni muhimu ili watu waweze kuishi pamoja wakati wowote na mahali popote

Kwa hiyo tuache kuwalaumu wengine,kusema uongo,kuwa na uhasama,hila,husuda,kashifa,na dhuluma. Tuiumbe upya jamii kwa maadili na tuyaendeleze maadili.Tuwe na maadili endelevu,Kuunda kitu,hiyo ni kazi ndogo,lakini kukifanya kitengemae,kishikamane,kiendelee,hiyo ni kazi kubwa zaidi.

Unajivuna ewe mtu kwa vile ni tajiri?Kwa nini?Kwa sababu utajiri wanakuwa nao hata wanyang'anyi na wezi na wauaji,na mashoga wanaume na makuadi,na kila aina ya watu waovu.Kwa nini basi uwe na majivuno?

Tutazame mambo anayofanya tajiri,au tuseme,yule anayetumia utajiri vibaya.Anapora mali za watu wengine,anadhulumu,anafanya udhalimu. Tazama starehe zao;-mapendo kinyume na maumbile kati ya wanaume,ushirikina,kuwekeana sumu katika chakula au katika vinywaji-haya yote si yanaletwa na fedha?

Usifikiri kwamba kwa vile matajiri hawaadhibiwi hapa,ina maana kwamba hawatendi dhambi.Kwa sababu,kama ingekuwa ni rahisi kuwaadhibu matajiri kwa hakika ungeona kwamba jela zimejaa wao.

Lakini pamaoja na maovu yake mengine mengi,utajiri una ovu hili pia,kwamba yeye aliye na utajiri,na anatenda maovu bila kujali,hawezi kamwe kuzuiwa kufanya hivyo, mpaka yamfike majeraha yasiyo na tiba,na hakuna mtu yeyote anayeweza kumwekea lijamu.
Kwa hiyo Budha anasema tusiogope kufa.Dini zote zishirikiane kuondoa maovu.Mtu akiogopa kufa anakuwa kama mtumwa,Yuko tayari kuvumilia kitu chochote kwa vile hataki kufa.Watu wanaishi maisha yao wanaogopa kifo kiasi kwamba wanashindwa hata kufaidi maisha yao.

Tuelimishane wote,hata kama wewe siyo hodari wa kuzungumza kwenye jukwaa.Unaye mtoto wako,una jirani,una rafiki, unaye kaka,ongea nao.Hata kama huna

akiba ya mawazo lakini unaweza kuongea mambo ya kawaida.Hakuna mtu asiyeweza kuongea mambo ya kawaida.

Dini zote lazima tushirikiane.Tusiwe na haraka ya kufanya mambo ya hatari,kwa sababu hiyo itakuwa siyo hekima.lakini tukiingizwa katika hatari na kama tunao wajibu wa kufanya hivyo,tukikimbia ,huo ni uoga.Lakini iwapo tutaitwa na viongozi ambao tunawaamini,tusikatae.Au labdawewe unafikiria kwamba tunatakiwa kwenda vitani kwa ajili ya kutetea "Uhuru","Usawa,""Demokrasi",na mengineyo,ambayo ni maneno tu matupu. Kama kuna viongozi watu wataenda vitani,siyo vingine.Vitani lazima awepo kamanda wa platuni na kamanda wa kombania.,siyo kama watu wanakwenda vitani tu. Lakini katika hali za kawaida,wakati hakuna ulazima,au sababu au shida yoyote,ambapo tunaamriwa na viongozi wa uhakika,tusiwe na haraka kufanya hivyoKwa sababu itakuwa ni kama kujionyesha tu na kufanya mambo ya kibinafsi.

Lakini yakitokea mambo yoyote yale ya kuwahatarisha viongozi wetu,basi hata kama itakuwa ni lazima kuvumilia vifo elfu,tusikatae kitu chochote.Usijiingize katika matatizo wakati ule unapoona kwamba mambo yanakwenda vile vile unavyopenda wewe.Kwa nini ujiletee hatari nyingi bila faida yoyote?

Jiepushe na vishawishi.Jitayarishe kama askari hodari.Mikono yako na miguu yako inahitaji kinga,lakini,kama mwanzo,siyo mikono hii au miguu hii;-ila ile mingine ya rohoKinga ya mikono ni kutenda matendo mema au matendo ya zaka.Kinga ya miguu ni kwamba isitembee mahali ambapo haitakiwi kutembea.

Usilie watu wanapokufa,kwani kama wameishi vyema ,hawana kitu cha kuhofu.Wakati wa kulia ni wakati tu unaungama dhambi zako.Ungama jioni dhambi ulizotenda asubuhi.Asubuhi ungama makosa uliyofanya usiku.Labda usiku hukufanya kitu chochote,labda ulikuwa umelala tu.Lakini,katika ndoto yako,kama kilikuwepo kitu chochote ambacho hakikutendeka kufuatana na maadili,kama hakikuwa sawa,au labda kilikuwa sawa lakini siyo sawa kabisa,basi ungama.

Hebu tuichunguze pamoja hii njia ya toba,ingawa nina hakika kwamba umechoka kabisa na ungependa kwenda kupumzika

Jambo la kwanza kabisa tulilaani lile tendo la uovu tulilolifanya.Halafu tuwe na unyenyekevu na moyo mkunjufu,Jambo la tatu tuwe na sala,na,bila kusahau,machozi,machozi usiku na mchana.Mtu akisema samahani na akitokwa machozi,si ndio tunasema amesema samahani kweli?Inakuwaje bai wewe unamwambia Mungu kwamba unaona aibu kubwa sana kuhusu makosa uliyoyafanya,lakini Mungu haoni machozi kwenye macho yako?Kwa hiyo unaona sasa kwamba ni rahisi kabisa kwako kufanya toba.Jambo la nne,toa zaka. Zaka inaosha dhambi zako Zaka peke yake inaweza kuzindoa dhambi zako bila hata kufanya haya mambo mengine..Halafu usiwe na hasira moyoni dhidi ya wengine-samehe ili usamehewe.Jambo la sita,wale watu ambao wanatenda dhambi ile ile ambayo ulikuwa umetenda,kawafundishe ili waokoke,ili makosa yao yasamehewe Kwa sababu yule ambaye bado hajaiingia katika laana,lakini

ameikaribia,anaweza vile vile kuwa mbali kabisa na hiyo laana.Halafu jambo la saba,zungumza neno kumsaidia yule anayedhulumiwa haki yake.

DINI YA UHURU

Uhuru walio nao wafuasi wa Budha unastahili kuigwa.Wabudha wengine hawafahamu kuhusu uhuru huu.Uko uhuru kamili wa kuamua na kufikiri wenyewe kukubali au kukikataa kitu chochote. Hatulazimiki kukikubali kitu katika jina la dini au kwa umaarufu wa mwalimu fulani wa kidini au kwa vile tunadhania kwamba tunatakiwa kuifuata misahafu mitakatifu.,au njia za kale.Wabudha wanao uhuru wa kuchunguza wenyewe kauli yoyote na kuikubali au kuikataa kufuatana na uamuzi wao kwa kutegemea mantiki Wabudha huwa hawasemi wanakatazwa kufanya hili au lile .Huwa wanasema tu kwamba hawataki kufanya jambo fulani kwa sababu linaleta matatizo fulani,huzuni maumivu au vurugu mingoni wa umma wanaojaribu kufanya matendo ya maendeleo.Kinyume chake wanatenda matendo fulani sio kwa vile dini yao imewaomba kufanya hivyo,ila kwa vile wenyewe wamekuja kuelewa faida ya hayo matendo mema kwa faida yao na wengine

Hii ni dini ya uhuru abayo haimzuii mtu kufanya mambo kama yanafuata maadili na hayana madharaWabudha wanapewa uhuru kamili wa kuendesha mambo yao ya kifamilia kufuatana na misingi ile ile muhimu ya kidini.Kwa wasomi pia hii dini ni kama machimbo ya dhahabu ya kufanya utafiti wenye faida na wa kina wa saioklojia,falsafa,sayansi na sheria ya mbingu.Ubudha unashikilia utajiri mkubwa sana wa kibinadamu,na ni ufunguo wa kutumainika wa maendeleo yetu ya kiroho na wokovu wetu kutokana na mambo yote yanayoleta kero na hali ya waiwasi na mashaka miongoni mwa umma.Hii ndiyo maana Ubudha zaidi ya miaka 2500

Iliyopita,umeweza kupokelewa na umma katika sehemu nyingi za dunia bila msaada wa kisiasa.Wakati wa Budha watu waliyakaribisha na kuyapokea mafundisho yake kama maneno ya heri na muafaka ambayo yalistahili kupokelewa duniani kote.Na ndiyo maana wabudha wameieneza dini yao bila ugumu wowoye na bila unyonyaji wa aina yoyote au uadhalimu,

BUDHA ALIHUBIRI KUFUATANA NA UZOEFU WAKE MWENYEWE

Hii ndiyo dini pekee inayoelezea mambo kutokana na uzoefu wa binadamu,utambuzi,hekima na mwangaza,na sio kama ufunuo au kama amri iliyotolewa na mungu yoyote.Inathibitisha kwamba matatizo ya binadamu ni lazima wayaelewe binadamu wenyewe,kwa uzoefu na kwa kuendeleza thawabu ya juu kabisa.Ufumbuzi wa matatizo lazima upatikane kwa kuitakasa na kuiendeleza akili ya binadamu Kwa hiyo ni rahisi kuona kwa nini watu hawauiti Ubudha'dini',ila wanauita 'utu'Lakini utu ndio mwanzo wa kila dini. Budha hakujitangaza kama mkobozi mchawi. Mafundisho yake ni kwamba sisi tunaweza kujikomboa wenyewe.

Msimamo huu unaufanya Ubudha kuwa na mantiki kuliko dini zote Budha alielezea mateso ni nini,sababu ya mateso na jinsi ya kuyaondoa matesoNguvu za nje haziwezi kuondoa mateso.Furaha itatokea tu iwapo watu watifanyia kazi.

TABIA TATU

Tabia tatu za kila kitu katika mbingu hii zinaelezwa vizuri katika dini hii Hakuna kitu kinadumu milele.Hakuna kitu kinaridhisha.Hakuna kitu kinaweza kuhusishwa na nafsi yako moja kwa mojaLakini kwa ajili ya kuzubaa kwa watu,sio wengi wanaoweza kuyaelewa haya mafunzo.

CHANZO CHA MATATIZO YETU

Jambo lingine muhimu katika dini hii ni maelezo kuhusu chanzo kikuu cha matatizo ya binadamu;-kufuatana na Ubudha,tunakabiliana na matatizo mengi katika dunia hii kwa ajili ya uchu mkubwa sana wa kibinafsi uliopo ndani ya akili yetuAmeainisha kwamba upo uchu wa aina tatu;-uchu wa kutaka kuishi,uchu wa kutaka starehe;-na uchu wa kuondoa yote haya;-uchu wa tatu ni uchu wa mtawa,au mtu yeyote anayetaka kujiepusha na matatizo kwa kutaka asiishi,sio kwa kujiua na kuyakimbia matatizo,ila kwa kuyashinda matatizo.Uchu huu wa aina tatu ndio unaosababisha tuishi,tuzaliwe tena.na maelfu ya matatizo mengine na heka heka za akili

Wanafalsafa na wanasaikolojia maarufu wa dunia nao pia wamezielezea hizi nguvu tatu.lakini wameziita kwa majina tofauti. Mwandishi wa Kijerumani Arthur Schopenhauer alizieleza hizi nguvu tatu kama uzazi,kujidumisha,na kujiua.Saikolojisti wa Austria Sigmund Freud alizieleza hizo hizo kama libido(nguvu ya ngono);-ego instinct,nguvu ya kujipenda;-na,death instinct,hamu ya kujiua.Aliyekuwa ni mwanafunzi maarufu wa Freud,Carl Jung alisema ‘kutokana na hizi nguvu,unakuwepo uwezo wa kuumba’Hivyo ndivyo wasomi wakubwa walivyo tayari kuunga mkono mafundisho ya Budha aliyofundisha karne ishirini na tano zilizopita Lakini tukiyatazama maelezo ya wafikiriaji wa sasa,tunaweza kuona kwamba Bhdha aliweza kuvuka kwa mbali ufahamu wao mdogo.

CHANZO CHA MATESO maswali na majibu

Ni dhahiri kwamba dunia inayo mateso tofauti kama vile kufa,kuoza,majonzi,kilio,maumivu,kukata tamaa na mengineyo,Budha alieleza kwamba kuzaliwa(jati)kunaleta mateso.Kama hakuna kuzaliwa,hakuna nafasi ya mateso kujipenyeza.

Q.Kwa nini kuna kuzaliwa?
A.Maisha,kama muungano wa mwili na akili,unasababisha kuzaliwa.Kwa maneno mengine,inapokuwepo dhana ya maisha(bhava)katika akili,kuzaliwa kunatokea
Q.Kitu gani kinasababisha muungano wa akili na mwili?
A,Mawazo yenye tamaa yanasababisha matendo ya tamaa,nahuo ndio muunganao wa mwili na akili

Q.Kitu gani kinaleta kung'ang'ania?
A.Uchu(tanha) ubasababisha kung'ang'aia
Q.Kitu gani kinasababisha uchu?
A.Hisia(vedana) zinasababisha uchu,
Q.Kitu gani kinasababisha hisia?
A.Mgusano wa hisi sita unasababisha hisia.
QKwa nini kunakuwepo mgusano wa hisi sita?
A.Misingi sita ya hisi inasababisha mgusano
Q.Misingi sita ya hisia inatokea vipi?
A.Muungano wa akili na mwili ubasababisha misingi ya hisi sita.
Q.Muungano wa akili na mwili unatokea vipi?
A.Inapokuwepo akili ambayo imedumaa(vinnana au vipaka citta)ndipo muungano wa akili na mwili unatokea.
Q.Akili iliyodumaa inatokea vipi?
A.Inaletwa na nguvu za vitendo ambazo bado hazijaanzishwa.
QNguvu za vitendo ambazo hazijaanzishwa inatokea vipi?
AKutokea kwake kunasababishwa na ujinga(avijja) ambao nikipegele cha tanha.

Kwa hiyo ni dhahiri kwaba ujinga(avijja) ndio msingi wa kuzaliwa na kuanza.Lakini huu ujinga sio chanzo hasa ila ni sharti linalokuwepo ili maendeleo yatokee.Matatizo mengi katika dunia hii ni kwa ajili ya uchu mkubwa sana wa kibinafsi. Kwa kutegemea kitu kimoja,kingine kinaweza kutokea. Hii ndiyo inaitwa paticca samupada,kutokea kwa kitu kimoja,kwa kutegemea kitu kingine.Mwenendo wote unaitwa gurudumu la maisha au bhava cakka. Kiungo kimoja kinaunganika na kiungo kingine Hivi viungo(kama vile,ujinga,vitendo na heka heka za akili) vinaitwa spoku kumi na mbili za gurudumu la maisha.

Zaidi ya hayo,spoku hizi zinaungana na wakati wa zamani,wa sasa,na wakati ujao.Katika maisha yaliyopita ujinga na nishati ya vitendo inaonekana.Katika maisha ya sasa zipo akili za kupinga maendeleo,muungano wa akili na mwili,misingi sita ya hisi,mgusano,raha,uchu,kung'ang'ania,mazoea.Baadaye,yaani katika maisha yajayo, tunaona kuzaliwa upya na mateso yanayoambatana nako.Kwa jinsi hii gurudumu la maisha limeungana na vipindi vya zamani,vya sasa na vya wakati ujao.

Hapa tunayo dini ambapo tunaikuta misingi ya kweli ya dini ambayo inaweza kudumishwa bila kuyabadili mawazo yake muhimu au misingi yake muhimu wakati wowote,mahali popote na katika masharti yoyote.Lakini uwezo wa binadamu kuyathamini haya mafundisho unaweza kutoweka baada ya muda.Binadamu anaweza kupata taabu kwa kuishi kutokana na misingi hii katika nchi ambayo imaejaa rushwa.Lakini thamani ya mafundisho haya ya dhahabu itadumu na itathaminiwa na watu wenye ufahamu kila mahalli

Inatumainiwa kwamba maelezo yaliyotolewa hapa yatakuwa jibu linalolifaa kwa swali lililoulizwa,"Ubudha ni nini?"-na kwa nini Ubudha bado unahitajika.

END

****